African Court on Human and Peoples' Rights

Arusha, Tanzania
Website: www.african-court.org
Telephone: +255-27-970-430

**JUDGMENT SUMMARY**

**SHIJA JUMA DHIDI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OMBI NAMBA 028/2016**

**HUKUMU KUHUSU SIFA ZA KESI NA FIDIA**

**13 JUNI 2023**

**UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU**

**Jijini Arusha, tarehe 13 Juni 2023**: Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama) ilitoa hukumu katika kesi ya *Shija Juma dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*.

*Shija Juma* (Mlalamikaji) ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Taifa Lililoshtakiwa). Wakati wa kuwasilisha Ombi hili, alikuwa amefungwa katika Gereza Kuu la Butimba mkoani Mwanza, baada ya kupatikana na hatia ya ubakaji na kuhukumiwa kifungo cha maisha. Mlalamikaji alidai kwamba Taifa Lililoshtakiwa lilikiuka haki zake chini ya Ibara ya 7(1) ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (Mkataba) kwa kumnyima haki ya kusikilizwa na kwa kumtia hatiani kwa misingi ya ushahidi usiotegemewa. Alitafuta fidia ili kurekebisha madai haya ya ukiukaji.

Mahakama iliona kwamba, kwa mujibu wa Ibara ya 3 ya Protokali ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (Protokali), ilibidi, awali, iamue kama ilikuwa na mamlaka ya kusikiliza Ombi hili. Katika suala hili, Taifa Lililoshtakiwa lilizua pingamizi kuhusu mamlaka yake ya kuwa mwamuzi wa kutoa suluhisho. Mahakama iliamua kwamba ilikuwa na mamlaka ya kuwa mwamuzi wa kutoa suluhisho kwa sababu Mlalamikaji alikuwa ametoa madai ya ukiukaji wa haki zake zinazolindwa na Mkataba.

Ingawa vipengele vingine vya mamlaka havikupingwa na Taifa Lililoshtakiwa, hata hivyo Mahakama ilivichunguza. Kuhusu suala hili, Mahakama iliamua kwamba ilikuwa na mamlaka ya kibinafsi kwa kuwa, tarehe 29 Machi 2010, Taifa Lililoshtakiwa liliwasilisha Azimio lililotolewa chini ya Ibara ya 34(6) ya Protokali. Azimio hili huwaruhusu watu binafsi kuwasilisha maombi dhidi ya Taifa Lililoshtakiwa kulingana na Ibara ya 5(3) ya Protokali. Mahakama ilisisitiza kwamba hali ya Taifa Lililoshtakiwa kuondoa Azimio hilo tarehe 21 Novemba 2019 haikuathiri Ombi hili, kwa sababu Ombi lilipokelewa Mahakamani tarehe 7 Juni 2016. Mahakama pia ilisema kwamba ilikuwa na mamlaka ya muda kwa kuwa madai ya ukiukaji yalitokea baada ya Taifa Lililoshtakiwa kuwa mshiriki wa Mkataba, Protokali na kuwasilisha Azimio linalohitajika chini ya Ibara ya 34(6) ya Protokali. Mwisho, pia iliamua kwamba ilikuwa na mamlaka ya eneo, ikizingatiwa kuwa jambo hili lilitokea katika eneo la Taifa Lililoshtakiwa.

Chini ya Ibara ya 6 ya Mkataba, Mahakama inatakiwa kubainisha iwapo mahitaji ya ukubalifu, kama yalivyotolewa katika Ibara ya 56 ya Mkataba na Kanuni ya 50 ya Kanuni za Mahakama (Kanuni), yametimizwa. Kuhusu suala hili, Mahakama ilizingatia kwanza pingamizi iliyotolewa na Taifa Lililoshtakiwa kuhusu kutomaliza njia zote za ndani za kutafuta suluhisho. Kuhusu utumiaji wa njia zote za ndani za kutafuta suluhisho, Mahakama ilibainisha kuwa, Mlalamikaji alipatikana na hatia ya ubakaji tarehe 22 Julai 2010 na Mahakama ya Wilaya. Alikata rufaa kwa Mahakama Kuu, ambayo ilitupilia mbali rufaa hiyo tarehe 29 Oktoba 2014. Alikata rufaa tena katika Mahakama ya Rufaa, mahakama ya juu kabisa katika Taifa Lililoshtakiwa, ambayo ilitupilia mbali rufaa hiyo na kukubaliana na hukumu ya Mahakama Kuu katika uamuzi wake wa tarehe 19 Februari 2016. Kwa hiyo, Mahakama ilichukulia kwamba Mlalamikaji alikuwa amemaliza njia zote za ndani za kutafuta suluhisho na alitimiza mahitaji ya kanuni ya 50(2)(e) ya Kanuni hizo.

Ingawa masharti mengine ya ukubalifu hayakupingwa na Taifa Lililoshtakiwa, Mahakama ililazimishwa na Ibara ya 6 ya Protokali kuhakikisha kwamba yametimizwa. Kuhusu suala hili, ilisema kwamba, Mlalamikaji alikuwa ametambuliwa waziwazi kwa jina na hili lilitimiza Kanuni ya 50(2)(a) ya Kanuni hizo. Pia ilisema kwamba madai yaliyotolewa na Mlalamikaji yalikusudiwa kulinda haki zake kwa mujibu wa Ibara ya 3(h) ya malengo ya Sheria ya Kuanzishwa kwa Umoja wa Afrika na hivyo Ombi liliwiana na Kanuni ya 50(2)(b) ya Kanuni hizo. Zaidi ya hayo, Mahakama ilipata kwamba lugha iliyotumika katika Ombi hilo haikuwa ya kudhalilisha au yenye matusi kwa Taifa Lililoshtakiwa au taasisi zake kwa kutimiza Kanuni ya 50(2)(c) ya Kanuni hizo na pia kwamba Ombi hilo halikutokana na habari zilizosambazwa kupitia vyombo vya habari pekee na hil lilitimiza Kanuni ya 50(2)(d) ya Kanuni hizo. Ombi ambalo liliwasilishwa miezi miwili (2) na siku ishirini na moja (21) baada ya kumaliza kutumia njia za ndani kutafuta suluhisho lilionekana kuwa liliwasilishwa katika muda mwafaka. Mahakama pia iliridhika kuwa Ombi hilo halikuzua madai ambayo tayari yalikuwa yameshaamuliwa mbele ya mahakama nyingine ya kimataifa na hivyo masharti yote ya ukubalifu kama yalivyoelezwa katika Ibara ya 56 ya Mkataba na Kanuni ya 50(2) ya Kanuni hizo yalikuwa yamezingatiwa. Kwa hiyo, Mahakama iliamua kwamba Ombi hilo linakubalika.

Kuhusu sifa za kesi hii, Mahakama iliangalia kama Taifa Lililoshtakiwa lilikiuka haki za Mlalamikaji chini ya Ibara ya 7(1) ya Mkataba, wakati ilipodaiwa kumnyima Mlalamikaji haki ya kusikilizwa. Mahakama ilithibitisha kwamba Mlalamikaji alikuwa ameruka dhamana na hivyo alipatikana na hatia bila kuwepo mahakamani. Hata hivyo, baada ya kukamatwa, alipewa nafasi ya kueleza kutofika kwake wakati wa usikilizwaji wa kesi hiyo lakini alishindwa kumshawishi hakimu kuhusu sababu zake. Kwa hivyo, Mahakama iliamua kwamba mahakama za kitaifa zilizingatia viwango vya haki vya kesi na kutupilia mbali madai hayo.

Kuhusu dai kwamba Mlalamikaji alipatikana na hatia kwa misingi ya ushahidi usiotegemewa, Mahakama iliamua kwamba Mlalamikaji alipatikana na hatia kutokana na ushahidi wa mashahidi wa upande wa mashtaka ambao haujakanushwa. Kwa hiyo Mahakama iliamua kwamba utaratibu uliopelekea Mlalamikaji kupatikana na hatia haukufichua kosa lolote la wazi au upotoshaji wa haki unaohitaji uingiliaji kati wake. Kwa hiyo, madai ya Mlalamikaji yalitupiliwa mbali.

Mahakama, baada ya kugundua kwamba hakukuwepo na ukiukaji wa haki za Mlalamikaji, iliamua kwamba maombi ya Mlalamikaji ya kutaka kupewa fidia hayakuwa ya haki.

Kila Mdaawa aliamriwa kulipa gharama zake za kesi.

**Taarifa zaidi**

Taarifa zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na matini kamili ya hukumu ya Mahakama ya Afrika, inaweza kupatikana kwenye tovuti katika: https://www.african-court.org/cpmt/details-case/0282016

Kwa maswali mengine yoyote, tafadhali wasiliana na Masijala kwa barua pepe registrar@african-court.org.

*Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama iliyoanzishwa na Mataifa Wanachama wa Umoja wa Afrika ili kuhakikisha kuna ulinzi wa haki za binadamu na watu barani Afrika. Mahakama ina mamlaka juu ya kesi na migogoro yote iliyowasilishwa kwake kuhusu ufasiri na matumizi ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu na hati zingine zozote zinazofaa za haki za binadamu zilizoidhinishwa na Mataifa yanayohusika. Kwa habari zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu katika www.african-court.org.*

.